# Kuhusu Huduma Ya Tujenge Nyumba Ya Mungu

**Tujenge Nyumba ya Mungu** ni huduma ya ***kimishenari*** inayojihusisha na ujenzi wa makanisa ya madhehebu ya ***Kipentekoste*** maeneo ya vijijini, kutoa misaada ya vyombo vya Injili pamoja na kusaidia wajane, watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu mijini na vijijini ili wafikie ndoto zao za kielimu.

## Madhumuni ya Huduma

Dhumuni kuu la huduma hii ni kusaidiana na wachungaji pamoja na washirika wao hususan katika maeneo ya vijijini ili kufanikisha ujenzi wa makanisa nchini *Tanzania ili watu walio na nia ya kumtafuta Mungu wamwabudu katika mazingira rafiki ya ibada.* Pamoja na jukumu hilo, huduma hii pia inatoa misaada ya vyombo vya Injili pamoja na kusaidia wajane, watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu mijini na vijijini ili wafikie ndoto zao za kielimu.

## Maono

Kueneza injili barani Afrika kwa njia ya majengo mazuri ya Ibada, vyombo vya mziki na kuwa mti wa kivuli kwa waliopoteza tumaini.

## Dhima

Kushirikiana na wachungaji na washirika wa makanisa ya madhehebu ya Kipentekoste maeneo ya vijijini katika kujenga makanisa, kutoa misaada ya vyombo vya mziki wa Injili pamoja na kusaidia wajane, watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu mijini na vijijini ili wafikie ndoto zao za kielimu.

## Madili ya Huduma

**Huduma hii imejengwa juu ya misingi ya kujitoa kusiko kwa kawaida; nia thabiti ya moyo wa kujitoa kwa kazi ya Bwana kwa njia ya mali zetu, elimu, ujuzi, muda na maombi bila kukoma kama alivyofanya Nehemia.**

## Upatikanaji wa Fedha

Vifuatavyo ni vyanzo vya fedha:

1. Michango ya hiyari kutoka kwa washirika wa huduma hii

2. Harambee zenye lengo la kutunisha mfuko wa huduma